

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA

Simu Na.: (026) 2333848, 2321607

2322853, 2322420

Nukushi: (026) 2322116, 2322146

2321013

Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa,

Barabara ya Mlezi,

S.L.P. 1923,

DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA
KIDATO CHA TANO NA VYUO VYA ELIMU YA UFUNDI MWAKA 2019**

Ndugu Wananchi,

Ofisi ya Rais – TAMISEMI inapenda kuwatangazia waliohitimu Wanafunzi waliohitimu Kidato cha Nne Mwaka 2018 na Wazazi/Walezi wa wanafunzi hao, kuwa Mchakato wa Uchaguzi wa Wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Elimu ya Ufundi umekamilika. Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano kwa mwaka 2019 wanatakiwa kuripoti kwenye Shule walikochaguliwa kuanzia **tarehe 8 hadi 22 Julai, 2019**. **Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti katika shule walizopangwa kwa wakati. Aidha, hakutakuwa na mabadiliko yoyote ya shule hadi Muhula wa Kwanza wa Masomo utakapokwisha.** Endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti shuleni hadi **tarehe 22 Julai, 2019 ambayo ndiyo siku ya mwisho ya kuripoti**, nafasi yake atakuwa ameipoteza na itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi.

Ndugu Wananchi,

Wanafunzi waliopangwa kwenye Vyuo vya Elimu ya Ufundi vilivyopo chini ya NACTE wanatakiwa: **kuthibitisha (confirm) kukubali kujiunga na kozi** zinazosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), kuanzia **tarehe 9 Juni, 2019 hadi 30 Agosti, 2019**. Mwanafunzi anawajibika kufanya uthibitisho kupitia kiunganishi kinachoitwa **Uthibitisho TAMISEMI** katika tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), ambayo ni **www.nacte.go.tz** ya **kukubali kuchaguliwa kwenye kozi na vyuo** walivyopangiwa. Mwanafunzi ambaye hatathibitisha kukubali nafasi aliyochaguliwa, nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine kati ya Wanafunzi wanaondelea kuomba kuchaguliwa katika vyuo hivyo kwa njia ya mtandao.

Ndugu Wananchi,

Wanafunzi wanaotaka kufanya mabadiliko ya kozi au vyuo walikochaguliwa, wanaruhusiwa kufanya hivyo kuanzia **tarehe 10 hadi 30 Agosti, 2019** kupitia tovuti ya NACTE.

Ndugu Wananchi,

Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano pamoja na **fomu za kujiunga** (joining instructions) zinapatikana kwenye tovuti ya OR-TAMISEMI ya **www.tamisemi.go.tz**. Mwanafunzi, mara uonapo jina kuwa umechaguliwa inabidi **upakue** fomu ya kujiunga na shule husika kwenye mtandao.

**Imetolewa na Katibu Mkuu,
OR-TAMISEMI**